# GRADE 6 MID TERM 2 MAY 2022

## KISWAHILI

# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

Wings 002

# GREDI 6 - 2022

## KISWAHILI : INSHA

Jina: ..............................................................................................

Jina la shule: ....................................................................................

| Viwango vya kutathmini | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kuzidisha matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
| Kuandika | 9 - 10 | 6 - 8 | 3 - 5 | 0 - 2 |

***Kuandika (Alama 10)***

**SIKU YA MICHEZO SHULENI**

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

# TARGETER WINGS

## KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

Wings 002

# GREDI 6 - 2022

# SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina ..............................................................................................................................

Jina la shule ..................................................................................................................

*Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi.*

| Jumla ya alama = 50 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango vya kutathmini | | | | |
| | Kuzidisha matarajio | Kufikia matarajio | Kukaribia matarajio | Mbali na matarajio |
| Kusikiliza na Kuzungumza | 5 | 3 - 4 | 3 | 0 - 2 |
| Kusoma kwa sauti | 91 | 61 - 90 | 31 - 60 | 0 - 30 |
| Ufahamu | 13 - 15 | 9 - 12 | 5 - 8 | 0 - 4 |
| Sarufi | 19 - 20 | 10 - 18 | 6 - 9 | 0 - 5 |

## SEHEMU YA KWANZA

I. **Kusikiliza na kuzungumza** (Alama 5)

***Jibu maswali utakayoulizwa na mwalimu.***

1. Mtu anayehusika katika kucheza mchezo akiwa mshiriki huitwaje?

   ____________________

2. Je, ni mchezo gani unaohusisha washiriki kumi na mmoja kwa kila timu na uhusisha miguu?____________________________

3. Michezo ina manufaa gani kwetu? Eleza __________________________

4. Taja mchezo mmoja ambao unahusisha kukimbia. ___________________

5. Ni mchezo gani ambao huiletea nishani nyingi nchi yetu?

   _________________________________

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## II. KUSOMA KWA SAUTI (Alama 10)

***Soma kifungu kifuatacho kwa sauti mwalimu akisikiliza.***

Siku moja Kombo aliamua kupeleka posa kwa wazazi wa mchumba wake. Kwa hivyo alimwalika Mtinda aandamane naye kwa wakweze. Safari ilipofika walijikwatua na kuanza safari yao.

Walipokaribia nyumbani kwa mchumba wake Kombo, walilakjwa kwa shangwe na wasichana wenyeji wao. Kila aliyewaona wavulana hao, aliwafurahia na kuwapokea kwa mikono miwili.

Kati ya wasichana waliowapokea, mmoja alikuwa mrembo sana. Mtinda kwa tamaa yake alimtamani sana na kummezea mate. Kabla ya chakula kuletwa wageni walijuana. Hapo ndipo Mtinda alipogundua kuwa yule msichana mrembo ndiye aliyekuwa mchumba wa rafikiye. Kutokana na tabia yake aliamua kuuvunja uchumba wa rafiki yake.

## III. UFAHAMU. (Alama 8)

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Mwanangu kimbia hapa, kando yangu hebu keti,
Nina nasaha ya kukupa, hata kama sina vyeti.
Si elimu ya kukopa, kama ile za tovuti.
***Nisikilize mwanangu, si wengi wakupendao.***

Amka mapema mwana, epukana na uvivu,
Na dadako andamana, shambani lima kwa nguvu,
Shuleni kasome sana, pia uwe mtulivu,
***Nisikilize mwanangu, si wengi wakupendao.***

Ukipata kibarua, kakifanye kwa juhudi,
Usiwe wa kubagua, ama uwe mkaidi,
Likija hili chukua, sitegemee ahadi,
***Nisikilize mwanangu, si wengi wakupendao.***

Uwe na nyingi huruma, cha kwako kitakufaa,
Usije kuwatengama, hata wale wano'chawa,
Mate usije kutema, hata kidharauliwa,
***Nisikilize mwanangu, si wengi wakupendao.***

**(a)** Shairi hili ni la aina gani? ______________________ (alama 1)

**(b)** Je, kwa nini mshairi anataka mwana aketi kando yake? (alama 1)

______________________________________

**(c)** Unawezaje kuepuka uvivu nyumbani? ____________________ (alama 1)

(d) Je, ubeti wa tatu unatuonya kutofanya nini? (alama 1)

______________________________

(e) Tambua na uandike mshororo unaorudiwarudiwa katika shairi hili.(alama 1)

______________________________

(f) Kulingana na shairi hili, mwanafunzi anapaswa kuwa na tabia gani shuleni?

______________________________ (alama 1)

(g) Neno **'kibarua'** katika ubeti wa tatu lina maana gani?

______________________________ (alama 1)

(h) Malenga anasisitiza bidii kwa nini? ______________________________ (alama 1)

**<u>UFAHAMU</u> (Alama 7)**

**<u>Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali.</u>**

Fisi aliamka asubuhi na kwenda kwa Simba. Alibisha mlangoni kwa robo saa hivi. Simba alipofungua mlango, Fisi alitabasamu na kumwambia, "Rafiki yangu bwana Simba, je, wafahamu kuwa wanyama hawakutambui kama mfalme wao?"

Simba hakufurahishwa na habari hizo. Alikasirika sana. Hata hivyo, kabla ya kumchukulia yeyote hatua kali, aliamua kuthibitisha madai ya Fisi. Aliondoka moja kwa moja hadi kwa duma, akamwuliza, " Ni nani mfalme wenu?"

"Ni nani hajui ni wewe?" Duma alisema kwa hofu. Simba aliwauliza wanyama wengine nao wakampa jibu sawa na lile la Duma. Majibu hayo yakampa matumaini na furaha tele moyoni. Akajiambia, "Hakuna mnyama awezaye kunipinga." Alipokuwa akiendelea kujipiga kifua, Ndovu akapita karibu naye akienda kunywa maji mtoni.

"Usinywe maji hayo kwanza, Ndovu. Je, unajua ni nani mfalme wa wanyama wote hapo mwituni?" Simba alimwuliza kwa matarajio makubwa.

Ndovu aliingiza mkonga wake majini, akaujaza maji na kumrushia Simba. "Ukifanya jinsi ambavyo nimefanya, basi wewe ndiwe mfalme," Ndovu alisema.

(a) Kwa nini Fisi alienda kwa Simba asubuhi? (alama 1)

______________________________

(b) Simba alipokea ujumbe wa Fisi namna gani? (alama 1)

______________________________

(c) Kwa nini jibu la Duma lilimfurahisha Simba? (alama 1)

______________________________

(d) Simba alimkataza Ndovu asinywe maji kwa kuwa (c 1)

______________________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

(e) Je, ni wanyama wote wanaotambua kuwa Simba ni mfalme wao? Eleza
________________________________________ (alama 1)

(f) Wanyama wangapi waliotajwa katika ufahamu? ______________ (alama 1)

(g) Je, jina jingine la Ndovu ni ______________________________ (alama 1)

## IV. SARUFI. (Alama 20)

1. **Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze vihasho kwa kutumia maneno yaliyo katika jedwali.** (alama 5)

**hulazwa, muuguzi, anapougua, wadi, kila**

Kwa kawaida ________ mtu _______ hupelekwa hospitalini kwa matibabu. Ugonjwa unapomzidia ________ kwenye _________ humo hospitalini. ________ ndiye humtunza akiendelea kupokea matibabu.

2. Tunga sentensi ukitumia nahau 'penga kamasi.' (alama 2)
________________________________________

3. ***Tambua kivumishi cha sifa katika sentensi:*** (alama 1)
Mpishi hodari hupika chakula kinachovutia ____________________

4. ***Kamilisha sentensi ukitumia kiwakilishi mwafaka:*** (alama 1)
Wakulima wanapalilia mihogo ____________________

5. ***Jibu maamkuzi:*** Hujambo? ________________________ (alama 1)

6. Yapange maneno haya jinsi yanavyotokea kwenye kamusi. (alama 2)
*i) mchezo ii) mcheshi iii) mchezeshaji iv) Mchezaji*
________________________________________

7. Tambua kivumishi cha idadi kutoka tunda hili. (alama 1)




________________________

8. ***Andika wingi wa:*** (alama 2)
Zizi ambalo lilijengwa ni la kuhifadhi mbuzi.
________________________________________

9. ***Kamilisha methali:*** (alama 2)
Achanikaye kwenye mpini ______________________

10. ***Chagua neno sahihi kutoka kwenye mabano ukamilishe sentensi:***
Mwalimu alileta _______cha barua kutoka posta. **(kitita, kipeto)** (alama 1)

11. Daktari hutumia nini kupima joto? ________________________ (alama 1)

12. ***Tegua kitendawili:*** Ajenga ingawa hana mikono ____ ________ (alama 1)

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com